
# MANISPAA YA TABORA YAFUNGUKA

TOLEO LA 02 | www.taboramc.go.tz |



HALIUZWI

# JENGO JIPYA LA UTAWALA MANISPAA YA TABORA

Manispaa ya Tabora ni yetu, tushirikiane kuijenga

tabora.mc | www.taboramc.go.tz | July-Sept-2022/2023

9 781405 234788

# YALIYOMO

1 Neno la Mstahiki Meya na Mkurugenzi

2 Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli za Kila Siku

3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

4 Matukio Katika Picha.

5 Bodi ya Wahariri.

# NENO LA MSTAHIKI MEYA NA MKURUGENZI



Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ni moja kati ya Manispaa chache sana Nchini ambazo zimebahatika kupata fedha nyingi sana za maendeleo katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa dhati kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais kwa kutupatia fedha nyingi sana za Miradi ya maendeleo katika sekta takribani zote mathalani Afya, Kilimo,Elimu pamoja na Miundombinu ya Barabara.

Katika Sekta ya Elimu Selikali ya awamu ya sita imetupatia Zaidi ya Bilioni tano ndani ya mwaka mmoja, ambazo zimejenga na kuboresha miundombinu ya Elimu Msingi na Sekondari,lakin vilevile fedha zingine zikienda kutekeleza sera ya Elimu bure pamoja na Malipo ya Wazabuni Mashuleni.

Kwenye Sekta ya Afya Manispaa ya Tabora imepokea Zaidi ya bilioni tatu ndani ya mwaka mmoja, ambazo zilielekezwa kwenye ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Afya kwa maana ya Hospitali ya Manispaa ya Tabora, Vituo vya Afya pamoja na Zahanati. Vilevile ikumbukwe Serikali kupitia Wizara ya Afya imeleta Vifaa tiba vingi sana katika Vituo vyetu hivi ambapo vina thamani ya Mabilioni ya fedha.

Na katika Sekta ya Miundombinu, Manispaa ya Tabora imepata fedha za kutosha kutoka Serikali kuu kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA). Barabara nyingi ambazo zilikuwa hazipitiki kwa sasa zinapitika na ukizingatia moja ya changamoto kubwa ilikuwa madaraja ambayo kwa sasa mengi yamejengwa na mfano mzuri ni Daraja la Kazima,linalounga barabara ya kutoka Kazima kwenda Ifucha.

Hivyo nitumie fursa hii pia kuwaomba wakazi wa Tabora kutumia neema hii kunufaika na miundombinu hii. Kipekee niwaombe wazazi kuwapeleka watoto wao Shule wapate elimu kwani Jamii ya Wanyamwezi bado kuna uchelewaji wa muitikio kwenye eneo hilo. Kwakuwa tupo vizuri kwenye maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023, niwaombe sana tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanaingia kwenye Madarasa mapya ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mhe. Samia Suluhu Hassan ambayo yana kila kitu ndani yake.

Mhre. Ramadhani S. Kapela
Mstahiki Meya
Halmashauri ya Manisaa ya Tabora.



Manispaa ya Tabora ni moja ya Halmashauri nane za Mkoa wa Tabora na ikiwa ni miongoni mwa Halmashauri 184 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo Manispaa ya Tabora ipo Makao Makuu ya Mkoa wa Tabora, hivyo kuipa fursa kubwa sana za kimaendeleo.

Kufuatia jitihada nyingi sana na za Makusudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna miradi mingi sana ya kimkakati ambayo inaufungua Manispaa ya Tabora na Mkoa wa Tabora kimaendeleo. Miongoni mwa Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa awamu ya tatu itokayo Makutupora-Tabora, Ujenzi wa Barabara mtandao wa Lami katika barabara kuu zinazounganisha Manispaa na Mkoa wa Tabora kwa ujumla ikiwamo barabara ya Nyahua-Chaya iliyokamilika hivi karibuni ikiunganisha Mikoa ya Tabora, Singida hadi Dodoma, Koga mpaka Katavi, na ile ya kuelekea Kigoma bado kipande kidogo kuunganisha na Tabora.

Serikali imeweza kuwekeza maji ya uhakika katika Manispaa ya Tabora na Mkoa wa Tabora kwa ujumla baada ya kutumia zaidi ya Bilioni Mia Sita kuleta Maji ya Ziwa Victoria, huku Manispaa ikiongeza Chanzo hiki cha maji kwenye vyanzo vyake vya awali ambavyo ni bwawa la Igombe na bwawa la Kazima.

Manispaa ya Tabora ina Umeme wa Grid ya Taifa, hivyo kufanya Nishati hii kuwa ya uhakika kwa matumizi ya Viwanda na Majumbani na sasa Manispaa inakuwa na uhakika wa kualika na kuhamasisha wawelkezaji kuja kuwekeza katika Manispaa ya Tabora kwakuwa sasa hivi mahitaji yote muhimu yapo na yanapatikana ikiwamo pamoja na Ardhi ya kutosha kuwekeza viwanda, ambapo Sera ya Manispaa ni kumpatia Ardhi bure muwekezaji mkubwa yoyote pamoja na Hati.

“Hivyo nitumie fursa hii kuwakaribisha wawekezaji wakubwa na wadogo kuja kuwekeza katika Manispaa yetu ya Tabora. Na napenda nitumie vilevile nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa upendeleo wake wa makusudi kabisa kutupatia fedha nyingi za maendeleo katika sekta karibia zote kwenye Hamlashauri ya Manispaa ya Tabora”,

DKT. PETER MAIGA NYANJA.
Mkugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Manispaa ya Tabora

# WAZIRI MKUU AMPONGEZA MKURUGENZI WA MANISPAA YA TABORA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa amempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Dkt. Peter M. Nyanja kwa usimamizi mzuri wa fedha za miradi ya Serikali.

Mhe. Majaliwa ametoa pongezi hizo katika ziara yake ya kikazi ya siku mbili Mkoani Tabora ambapo ambapo alitembelea na kukagua ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwamo jingo la Utawala la Manispaa ya Tabora

Aidha Mhe. Majaliwa katika kikao na Viongozi pamoja na Watendaji wa Mkoa wa Tabora amepokea Salamu za Mkoa wa Tabora kutoka kwa Mkuu wa Mkoa Dkt. Batilda Burian ambapo pamoja na mambo mengine amemshukuru sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa upendeleo wake mkubwa kwa Mkoa wa Tabora.

Kwani zaidi ya Bilioni mia moja na kumi (110) zimetumika kwenye miradi ya maendeleo Mkoani Tabora kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kwa upande wa Manispaa ya Tabora ikipata zaidi ya Bilioni nane (8) kwenye miradi yake maendeleo.

Katika Manispaa ya Tabora Mhe. Majaliwa amepata fursa ya kuongea na Wananchi naMhe.Kassim Majaliwa, Watendaji wa Serikali na kueleza namna gani Serikali ya awamu ya sita imejipanga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Na baadae amekagua mradi wa Jengo Jipya la Utawala linalojengwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu, Serikali ya awamu ya sita chini ya Uongozi imara wa Mama Samia Suluhu Hassan jingo ambalo kwa sasa liko hatua ya umaliziaji.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa amewataka Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Tabora kuwekeza kwenye miradi yenye tija, ya kimkakati na yenye kuleta matokeo chanya kwa mapato yao ya ndani,kwani miradi mingi inayotekelezwa ni midogomidogo na haina tija sana kwa Halmashauri husika.

Mhe.Kassim Majaliwa amewataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuongeza tija, ubunifu na mbinu za kukusanya mapato ya ndani ili waweze kutoa huduma bora kwa Wananchi. Vilevile amewataka kufuata sheria na taratibu za matumizi ya fedha hizo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zinapelekwa kwanza benki ndio zirudi kufanya matumizi.

Aidha katika kipengele cha mapato amesisitiza mawakala wapewe mikataba na ikiwa ni baada ya kufanya tathimini ya kina kwenye vyanzo husika, hii ikiwa ni kuleta ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

Aidha katika hotuba yake Mhe.Kassim Majaliwa amemtaka Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora kuhakikisha fedha zote ambazo hazijaingia kwenye



akaunti husika benki katika Halmashauri zote za Mkoa wa Tabora zinapelekwa haraka iwezekanavyo na vinginevyo achukue hatua muhimu ikiwa ni pamoja na kushirikisha vyombo vingine vya Serikali ikiwamo TAKUKURU.

Katika hatua nyingine Mhe. Majaliwa amemuagiza Katibu Tawala Mkoa wa Tabora Dkt. John Mbowe kufanya msawazo wa watumishi ndani ya Mkoa wa Tabora ikiwa ni kupambana na uhaba wa Watumishi kwani kuna Halmashauri zingine zinakuwa na watumishi wengi katika kada flani huku Halmashauri nyingine zikiwa na

uhaba mkubwa wa watumishi wa kada kam hiyo hiyo.

Waziri Mkuu amewaagiza Meya na Wenyeviti wa Halmashauri wawe wakali kwenye matumizi ya fedha za Halmashauri na wahakikishe taratibu na kanuni zinafuatwa ambapo ameeleza kwamba Baraza la Madiwani linawajibu wa kuhakikisha kwamba kila shilingi inatumika kulingana na bajeti iliyopangwa na sio vinginevyo, na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu zote zinafuatwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Dkt Peter Maiga Nyanja wakati akielezea utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jingo la utawala amesema kwamba mpaka sasa jengo linahitaji zaidi ya Bilioni mbili ili kuweza kukamilika kabisa, ambapo Mhe. Majaliwa ameahidi Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaipatia Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ili kuendelea kukamilisha jengo hilo kwa sababu Mkurugenzi na Manispaa ameweza kusimamia vyema matumizi ya fedha za awali.

Mwisho kabisa Mhe.Kassim Majaliwa amewashukuru Wananchi wa Tabora kwa mwitikio wao mkubwa kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lakini vilevile kwa ukarimu wao na mapokezi makubwa wakati alipokuja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Samia Suluhu Hassan na kusisitiza kwamba upendo wa watu wa Tabora unawapa nguvu wao kama Viongozi wa Serikali.

# DKT. NDUGANGE ASHAURI UJENZI WA SHULE MPYA UZINGATIE MIUNDOMBINU YA MICHEZO

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (AFYA) Dkt. Festo Dugange, ameagiza ujenzi wa shule mpya za sekondari na msingi uzingatie miundombinu ya michezo kwa wanafunzi. Aidha amezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya michezo wanapopanga na kupim miji yao ili iendane na mahitaji ya wakati husika.



Akifunga mashindano hayo ya UMISSETA na UMITASHUMITA TAIFA 2022 Dkt. Dugange amesema kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa michezo na ndiyo maana imeamua kuendeleza kwa wanafunzi hao kushiriki ili kuendeleza vipaji vya watoto hao.

Aidha kuhusu suala la upungufu wa waalimu wa masomo ya michezo Dkt. Dugange alisema anawahakikishia kuwa Serikali imejipanga kuongeza ajira za kada ya ualimu kwa masomo yote wakiwemo waalimu wa michezo kwa sahule za msingi na sekondari.

Na katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za michezo, Sanaa na utamaduni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Serikali imeanzisha Kitengo cha Utamaduni, Sanaa na Michezo kuanzia Julai 1, 2022.

“Changamoto za Halmashauri kutokuwa na Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo Ofisi ya Rais – TAMISEMI tutashirikiana na wizara ya Utamaduni , Sanaa na Michezo na Wizara ya Utumishi ili kuzifanyia kazi changamoto hizo zilizopo na Kitengo hiki kuimarika ili kuzifanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Sita,” alisisitiza Dkt.

Dugange.

Kando nae, Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dkt. Batilda S. Burian ameishukuru sana Serikali ya Awamui ya Sita kwa kuamua kuuchagua Mkoa wa Tabora kuwa mwenyeji wa mashindano hayo, na kwamba michezo hiyo imekuwa na tija kubwa sana kwa wanafunzi wenyewe, waalimu imleta furaha kubwa miongoni mwao na kuimarisha upendo sambamba na kuinua uchumi wa Mkoa kwa ujumla kwani wajasiliamali wadogowadogo, wakubwa na wote kwa pamoja wamefanikiwa kufanya biashara zao vizuri kabisa.

Kufungwa kwa mashindano haya, kunafungua fursa nyingine ya mashindano kwa shule za msingi Afrika Mashariki yatakayoanza mwishoni mwa mwezi huuwa Agosti katika Jiji la Arusha.

# UZINDUZI WA MIONGOZO YA ELIMU MANISPAA YA TABORA

Manispaa ya Tabora ikiwa ni miongoni mwa Halmashauri zilizopo Nchini imezindua rasmi Miongozo na mikakati ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya Elimu Msingi na Sekondari. Uzinduzi huu umeshuhudiwa na wageni na Viongozi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Shule za Sekondari, Walimu wakuu wa Shule za Msingi, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu, Madiwani , Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Dkt. Peter Maiga Nyanja pamoja na Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhani Kapera.



Serikali ya awamu ya sita imekuwa ikikabiliana na changamoto nyingi sana zinazowasibu Watanzania. Sekta ya Elimu nayo ni miongoni mwa Sekta zenye Changamoto nyingi sana na hivyo kuilazimu Serikali kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo ambazo ni pamoja na Uhaba wa Madarasa, uhaba wa Madawati, Upungufu wa Walimu pamoja na Vifaa vya kujifunzia.

Ofisi ya Rais TAMISEMI imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathimini ya mara kwa mara ili kuona maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Tathimini ya hivi karibuni imebaini uwepo wa mafanikio makubwa lakini pia baadhi ya Changamoto, hii ikiwa ni kutokana na Uwekezaji Mkubwa unaofanywa na Serikali ya Awamu ya sita kwenye Sekta hii hususani kumaliza uhaba wa madarasa, uhaba wa Walimu na uhaba wa Madawati.

Aidha Ofisi ya Rais –TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu katika kukabiliana na Changamoto zinazoikabili Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari Nchini, Imeandaa Zana kuu tatu za kuzingatiwa katika usimamizi na uendeshaji wa shule;

Changamoto katika Uboreshaji Elimu Msingi na Sekondari: Nini kifanyike?
Mkakati wa kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji ngazi ya Elimu Msingi na Sekondari.
Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa.
Mgeni Rasmi katika hafla hii ambaye ni Mustahiki Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhani Kapera amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassani kwa upendeleo mkubwa sana kwa manispaa ya Tabora hususani Sekta ya Elimu na kipekee sana amemshukuru Mhe. Rais kwa fedha zilizokuja hivi karibuni kwa ajili ya kujenga madarasa fedha zaidi ya bilioni moja milioni miatatu.

Mustahiki Meya amewapongeza Walimu wa Manispaa ya Tabora kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha Wanafunzi wanafaulu vizuri lakini vilevile

Miradi ya Maendeleo kwa fedha zinazoletwa na Serikali Mashuleni.

Mhe. Ramadhani Kapera ametanabaisha Manispaa ya Tabora ikiwa ni miongoni mwa Halmashauri zilizopo Nchini imezindua rasmi Miongozo na mikakati ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya Elimu Msingi na Sekondari. Uzinduzi huu umeshuhudiwa na wageni na Viongozi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Shule za Sekondari, Walimu wakuu wa Shule za Msingi, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu, Madiwani , Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Dkt. Peter Maiga Nyanja pamoja na Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhani Kapera.

Serikali ya awamu ya sita imekuwa ikikabiliana na changamoto nyingi sana zinazowasibu Watanzania. Sekta ya Elimu nayo ni miongoni mwa Sekta zenye Changamoto nyingi sana na hivyo kuilazimu Serikali kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo ambazo ni pamoja na Uhaba wa Madarasa, uhaba wa Madawati, Upungufu wa Walimu pamoja na Vifaa vya kujifunzia.

Ofisi ya Rais TAMISEMI imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathimini ya mara kwa mara ili kuona maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Tathimini ya hivi karibuni imebaini uwepo wa mafanikio makubwa lakini pia baadhi ya Changamoto, hii ikiwa ni kutokana na Uwekezaji Mkubwa unaofanywa na Serikali ya Awamu ya sita kwenye Sekta hii hususani kumaliza uhaba wa madarasa, uhaba wa Walimu na uhaba wa Madawati.

Aidha Ofisi ya Rais –TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu katika kukabiliana na Changamoto zinazoikabili Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari Nchini, Imeandaa Zana kuu tatu za kuzingatiwa katika usimamizi na uendeshaji wa shule;

Changamoto katika Uboreshaji Elimu Msingi na Sekondari: Nini kifanyike?
Mkakati wa kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji ngazi ya Elimu Msingi na Sekondari.
Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa.
Mgeni Rasmi katika hafla hii ambaye ni Mustahiki Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhani Kapera amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassani kwa upendeleo mkubwa sana kwa manispaa ya Tabora hususani Sekta ya Elimu na kipekee sana amemshukuru Mhe. Rais kwa fedha zilizokuja hivi karibuni kwa ajili ya kujenga madarasa fedha zaidi ya bilioni moja milioni miatatu.

Mustahiki Meya amewapongeza Walimu wa Manispaa ya Tabora kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha Wanafunzi wanafaulu vizuri lakini vilevile pongezi hizo zikaenda sambamba na usimamizi mzuri wa Miradi ya Maendeleo kwa fedha zinazoletwa na Serikali Mashuleni.

Mhe. Ramadhani Kapera ametanabaisha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora katika mwaka wa fedha unaokuja, Manispaa itaweka kipaumbele zaidi ujenzi wa Nyumba za Walimu na Manesi kwani kundi hili la Watumishi ni nyeti na ni kundi lenye watumishi wengi na linafaa kupewa kipaumbele sana kulingana na umuhimu wake mkubwa.

Aidha Mhe. Kapera amewasihi na kuwataka Wakazi wa Tabora wabadilike waweke elimu kuwa kipaumbele kwao. Amewataka watoe ushirikiano mkubwa kuhakikisha kuwa watoto wanakula chakula shuleni kwani shibe ni miongoni mwa sababu zinazochangia ufaulu kwa watoto. Hata hivyo amewataka Walimu na Waratibu Elimu Kata wasichoke kuwaelimisha Wananchi na kuendelea kuwahamasisha kuchangia chakula ili Manispaa iweze kuongeza ufaulu katika mitihani ya Kitaifa.

Nae Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Dkt. Peter M. Nyanja amewataka Wakuu wa Shule watoe Matangazo kwa Umma mara wapatapo fedha za Miradi ili Jamii nayo ishiriki vyema kwenye kujenga na kusimamia matumizi sahihi ya fedha hizo, lakini villevile jamii iweze kutambua ni kwa kiasi na kasi ipi Serikali ya Awamu ya Sita inaleta pesa kwenye miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Aidha Dkt.Nyanja ametumia fursa hii kuwaeleza Wakuu wa Shule kuwa kwa sasa kwa Shule zenye Miradi,kabla Mkuu wa

Shule hajaandika Muhtasari wa malipo analazimika kuwasiliana na Kiongozi wa Timu ya Ukaguzi na Ufuatiliaji ya Manispaa ili aweze kufika kwenye mradi husika na timu yake na kukagua kama ubora umezingatiwa kwenye mradi ikiwa sambamba na taratibu zote za Manunuzi kama zimefuatwa ndipo malipo yaendelea.

Aidha, Bi.Haika Masue, akimwakilisha Katibu Tawala wa Wilaya ya Tabora amesema Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imejipanga vyema sana kwaajili ya ufuatiliaji na Usimamizi wa fedha zote za Serikali zinazokwenda kwenye miradi ya maendeleo katika Sekta zote ndani ya Manispaa ya Tabora.

# DKT. MSONDE AAGIZA KUKAMILISHWA KWA WAKATI MIRADI YA ELIMU

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Dkt. Charles Msonde amewataka Maafisa Elimu Miko ana Maafisa Elimu Sekondari wa Halmashauri kusimamia miradi ya elimu kukamilika kwa wakati ili kuepuka kwa hoja za ukaguzi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Hayo yameelezwa leo tarehe 15 Agosti, 2022 Mkoani Tabora wakati akifungua kikao kazi cha Mafunzo na kujengewa uwezo kwa maafisa hao kuhusu Usalama wa Mazingira na Jamii katika kutekeleza mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (Tanzania Secondary Education Quality Improvement Project – SEQUIP) katika maeneo yao ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake.

Dkt. Msonde aliendelea kufafanua kuwa, Serikali imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya elimu na fedha za mradi wa SEQUIP na kuboresha elimu ya Sekondari, kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu, kupunguza vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kuacha shule, kuwasaidia wanafunzi kumaliza elimu bora ya sekondari na kupunguza changamotoza upatikanaji wa elimu nchini.

Dkt. Msonde amewataka maafisa hao katika kusimamia ujenzi wa shule hizo kuepuka migogoro ya ardhi inayoweza kutokea na kusababisha matatizo kwa kutoendelea kwa ujenzi. Aidha vilevile kusimamia ujenzi ili uendane na thamani ya fedha iliyotolewa , pia pia kusimamia utekelezaji wa ujenzi unaoweza kuzingatia muda uliowekwa ili ukamilike kwa wakati na shule hizo I;I ziweze kukamilika na wanafunzi kwa haraka.

“Ninyi ni wabobezi katika usimamizi na utekelezaji wa elimu tushirikiNaibu Katibu Mkuu (Elimu) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Dkt. Charles Msonde amewataka Maafisa Elimu Miko ana Maafisa Elimu Sekondari wa Halmashauri kusimamia miradi ya elimu kukamilika kwa wakati ili kuepuka kwa hoja za ukaguzi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Hayo yameelezwa leo tarehe 15 Agosti, 2022 Mkoani Tabora wakati akifungua kikao kazi cha Mafunzo na kujengewa uwezo kwa maafisa hao kuhusu Usalama wa Mazingira na Jamii katika kutekeleza mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (Tanzania Secondary Education Quality Improvement Project – SEQUIP) katika maeneo yao ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake.

Dkt. Msonde aliendelea kufafanua kuwa, Serikali imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya elimu na fedha za mradi wa SEQUIP na kuboresha elimu ya Sekondari, kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu, kupunguza vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kuacha shule, kuwasaidia wanafunzi kumaliza elimu bora ya sekondari na kupunguza changamotoza upatikanaji wa elimu nchini.

Dkt. Msonde amewataka maafisa hao katika kusimamia ujenzi wa shule hizo kuepuka migogoro ya ardhi inayoweza kutokea na kusababisha matatizo kwa kutoendelea kwa ujenzi. Aidha vilevile kusimamia ujenzi ili uendane na thamani ya fedha iliyotolewa , pia pia kusimamia utekelezaji wa ujenzi unaoweza kuzingatia muda uliowekwa ili ukamilike kwa wakati na shule hizo I;I ziweze kukamilika na

wanafunzi kwa haraka.

“Ninyi ni wabobezi katika usimamizi na utekelezaji wa elimu tushirikiane sote ili miradi hii iwe yenye kuleta tija katika Taifa letu,” alisema Dkt. Msonde.

Awali akitoa maelezo mafupi Mkurugenzi Msaidizi Idara Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais-TAMISEMI Bi Hadija Mcheka amemuelezaNaibu Katibu Mkuu Dkt. Charles Msonde kuwa , kikao hicho kitakuwa cha siku mbili kwa kujengewa uwezo kwa maafisa hao kwa kufundishwa mada mbalimbali kutoka kwa wataalamu ili kupata ufahamu taratibu za usimamizi wa mradi na kupata nafasi ya kutoa maoni katika kufanikisha mradi unatekelezwa kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande wake Afisa Elimu Mkoa wa Tabora Bw. Juma Kaponda akiongea kwa iaba ya watendaji hao ameishukuru sana Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya elimu na kuahidi kusimamia kwa kutekeleza na kufuata sheria, miongozo na taratibu zinazowataka kwa kuhakikisha Sekta ya elimu inakuwa na manufaa kwa Taifa.



# MUSTAHIKI MEYA,MKURUGENZI NA WADAU WAKUBALIANA MIKAKATI NA MUDA WA KUJENGA MADARASA 69

Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora Dkt. Peter Maiga Nyanja akiambatana na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhan Shabani Kapela pamoja na wadau wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 69 wamekutana na Wakuu wa Shule za Sekondari hususani Shule ambazo zimepata fedha za madarasa kutoka Serikali kuu kwa ajili ya kuweka mikakati ya kujenga vyumba vya madarasa 69 ya kidato cha kwanza vyenye thamani ya Tzs. 1,380,000,000/= (Bilioni Moja, na Milioni Mia tatu themanini tuu) ikiwa ni mgawo kwa Manispaa ya Tabora ambapo uwiano wa darasa moja kwa milioni ishirini.



Kikao hicho kimefanyika katika ukumbi wa Manispaa, ambapo kimejumuisha wadau wote wa Ujenzi wakiwamo Mafundi ujenzi, Wazabuni, Watendaji Kata, Mafundi wa thamani, Wakuu wa Shule ,pamoja na Menejimenti ya Manispaa ya Tabora. Aidha Wadau wamekumbushwa kuwa kufikia January shule zinapofunguliwa watoto wa kidato cha kwanza wanatakiwa kutumia madarasa haya.

Aidha katika kikao kazi hiki, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe. Ramadhani Kapela kwa nafasi yake amesisitiza kuwa kila mradi uwe na fundi mmoja, na fundi mmoja asiwe na miradi miwili kwani kufanya hivo kutapunguza kasi ya utekelezaji wa mradi na kuchelewesha kazi.

Vilevile Mstahiki Meya amewataka Watendaji Kata hususani kwenye vikao vyao vya WDC wawahimize Wananchi kushiriki na kuweka nguvu zao kwenye miradi hii kazi ya kuchimba msingi na kuweka kifusi na mawe kwenye msingi iwe sehemu ya nguvu kazi zao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora Dkt. Peter Nyanja katika maelekezo yake amewataka Wakuu wa Shule waunde Kamati za ujenzi na ununuzi kwa kufuata miongozo inavyotaka na kusisitiza wanakamati hao pindi wanapopatikana wapewe mafunzo ya kuwawezesha ili wafanye shughuli zao kwa weledi mkubwa.

Dkt. Nyanja amewataka Wakuu wa Shule kuleta taarifa ya utekelezaji kwa kila hatua ya ujenzi kabla ya malipo kufanyika na kuongeza kuwa baada ya hapo atatuma timu yake ya ukaguzi kwenda kukagua ubora wa mradi kwa hatua hiyo lakini vilevile kupata thamani halisi ya malipo yanayoombwa.

Vilevile Mkurugenzi amewaomba Mawakala wa vifaa vya ujenzi wawe waadilifu na wazalendo, wasitumie mwanya huu kupandisha bei za vifaa vya ujenzi hususani saruji, nondo, bati nk ambavyo ndio vifaa muhimu sana kwa ujenzi wa madarasa. Aidha Mkurugenzi ametumia fursa hiyo kuwaomba wazabuni wa madini ya ujenzi kutopandisha bei ya madini hayo kwa kivuli cha ujio wa fedha hizi za madarasa.

Aidha Dkt.Nyanja amewataka mafundi ujenzi kuongeza ubunifu na jitihada katika kazi zao na amesema hategemei kukuta ukuta ama sakafu imepasuka kwa sababu yeyote ile ya kiufundi, huku akiongeza kuwa mafundi milango watumie Mbao kavu za miti migumu lakini vilevile milango na madawati vipigwe Vanishi na Msasa kabla ya kukabidhiwa.

Katika kuhitimisha kikao kazi hiki, wajumbe wote waliohudhuria wamekubaliana kwa pamoja kuwa ujenzi uanze rasmi mnamo tarehe 16 mwezi October na ukamilike kufikia tarehe 15, mwezi Disemba mwaka huu

# MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA INAYOENDELEA KUTEKELEZWA MANISPAA YA TABORA



*Mwonekano wa mbele wa Jengo Jipya la Utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, jengo liko linaendelea kujengwa katika hatua ya umaliziaji.*



*Mwonekano wa nyuma wa Jengo Jipya la Utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Jengo linaendelea kujengwa likiwa hatua ya umaliziaji.*



*Madarasa natatu na ofisi mbili,zilizojengwa kwa fedha za UVIKO-19 ,Shule ya Sekondari Ndevelwa,Manispaa ya Tabora,Mkoa wa Tabora.*



*Madarasa Mawiili na Ofisi moja, Madarasa yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO-19, Shule ya Sekondari Kazima.*




*Muonekano wa mbele wa Jengo la Utawala la Hospitali ya Manispaa ya Tabora*



*Picha ikionesha baadhi ya Majengo ya Hospitali ya Manispaa ya Tabora mathalani Jengo la Wagonjwa wa Nje(OPD), Jengo la Mama na Mtoto pamoja na Jengo la Maabara.*



*Picha ikionesha madarasa, maabara, jengo la Utawala  pamoja na Maktaba katika Shule ya Sekondari Mpera, Shule ambayo imejengwa kwa fedha za Wahisani na Wadau wa Maendeleo kupitia mradi wa SEQUIP.*



*Picha hii inaonesha jengo la Wagongwa wa Nje (OPD) la Kituo cha Afya Misha, Kituo ambacho kimejengwa kwa fedha za TOZO kwa thamani ya shilingi za Tanzania milioni miatano (500,000,000/).*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mhe. Samia Suluhu Hassan wa saba kutoka kulia akikata utepe kuzindua rasmi barabara ya Nyahua-Chaya Mkoani Tabora, Barabara inayounganisha Mikoa ya Tabora na Singida kupitia Wilaya ya Itigi. Ufunguzi huu umefanyika 17 May,2022.*



*Mustahiki Meya wa Manispaa ya Tabora Mhe.Ramadhani Kapera akimkabidhi tuzo ya ngao pamoja na pesa taslimu kiasi cha Tsh.Milioni tatu Afisa Maendeleo Bi Tumaini Mgaya kwa kuwa Mfanyakazi Hodari naMbunifu.*



*Mhe.Ramadhani Kapera,Meya wa Manispaa ya Tabora akipokea Mwenge wa Uhuru mnamo tarehe 04/08/2022 ambao ulikimbizwa Manispaa ya Tabora na kuzindua miradi yenye thamani ya Tsh.3,037,314,970/=*



*Bi. Hppyness Nnko, Afisa Kilimo na Umwagiliaji Manispaa ya Tabora akipokea zawadi ya tuzo na cheti kutoka kwa Mhe.Thobias Andengenye,Mkuu wa Mkoa wa Kigoma akiambatana na Balozi Dkt. Batilda Buriani,Mkuu wa Mkoa wa Tabora,ikiwa ni zawadi za kufanya vizuri na kuibuka kidedea katika maonesho ya nanenae ya kanda ya Magharibi mwaka 2022, yaliyofanyika viwanja vya Ipuli Manispaa ya Tabora.*



*Bi.Haika Masue,Afisa Tarafa ya Tabora Kaskazini,Akimwakilisha Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tabora Katika Uzinduzi wa Chanjo ya Polio awamu ya tatu,uzinduzi uliofanyika Agosti 30,2022. Kulia kwake ni Mkuu wa Sehemu ya Elimu Sekondari,Ndg.Nyahori Mahumbwe, na kushoto kwake ni Mganga Mkuu wa Manispaa ya Tabora Dkt.Baraka Msumi.*



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora Dkt.Maiga Nyanja(Mwenye shati ya bluu katikati) akiwakabidhi pikipiki 15 zenye thamani ya milioni thelathini na saba na laki tano(375000000/=) Vijana wa Kikundi cha Kazi iendelee cha kata ya Itonjanda pamoja na Vijana wa Kikundi cha Wakujiramba cha Kata ya Ng'ambo.Jitihada hizi ni ni katika kutekeleza sheria ya fedha ya kupeleka asilimia kumi (10%) ya mapato ya Halmashauri kwenye Vikundi vya Vijana, Wanawake na Walemavu..*

# BODI YA WAHARIRI

**DKT. PETER MAIGA NYANJA**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Manispaa ya Tabora**

**PAUL P. KASEMBO**
**Kaimu Mkuu wa Kitengo**
**Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini**
**Manispaa ya Tabora**

**ALEX E. SIRIYAKO**
**AFISA HABARI**
**Manispaa ya Tabora**

**OFISI YA MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**
**4 BR, KIWANJA CHA NDEGE**
**SLP 174**
**45182 TABORA**
**www.taboramc.go.tz**
**Barua Pepe : md@taboramc.go.tz**